

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE**



**TANGAZO LA NAFASI YA WALIMU KUHAMIA KATIKA SHULE MPYA ITAKAYOENDESHWA
KWA MFUMO WA LUGHA YA KIINGEREZA**

Tarehe: 14 Februari, 2022

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) katika Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale imeanzisha Shule Mpya ya Awali na Msingi itakayoendeshwa kwa mfumo wa lugha wa Kiingereza (Pre & Primary English Medium school) katika Kijiji cha Busengwa, Kata ya Kharumwa. Shule inatarajiwa kufunguliwa na kuanza masomo Mwezi March, 2022.

Hivyo, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inatoa Tangazo kwa Walimu wote walioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ambao tayari ni Waajiriwa wa Serikali na wenye uwezo wa kufundisha kwa mfumo wa lugha ya Kiingereza, wanao hitaji watume maombi ya kuhamia katika shule hiyo.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji lazima awe Mwalimu Mwajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.
- ii. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiingereza.
- iii. Barua ya maombi lazima ipitishwe na Mwalimu Mkuu, Afisa Elimu Kata na Afisa Elimu wa Wilaya.
- iv. Mwombaji aambatishe wasifu binafsi (CV) wa hivi karibuni.
- v. Maombi yaambatishe na nakala ya vyeti vya Elimu na Taaluma.
- vi. Mwombaji athibitishwe kujigharamia uhamisho wake kwenye barua ya maombi.
- vii. Maombi yote yaandikwe kwa,-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 352,
NYANG'HWALE – GEITA**

MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 23 FEBRUARI, 2022 SAA 9:30 ALASIRI

Imetolewa na;-

Husna Toni

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 352
NYANG'HWALE**